

# **Kiswahili katika karne ya 20 : chombo cha ukombozi, utafa na ukandamizaji**

**Jean de Dieu Karangwa**  
*INALCO, Paris*

Ikisiri

Historia ya Kiswahili katika karne ya 20 ni mada ambayo imechunguzwa na watafiti kadhaa katika miaka iliyopita. Orodha yao ikiwa ndefu, tutataja wachache miongoni mwao kama vile Whiteley (1969), Heine (1970), Chiraghdin na Mnyampala (1977), Polome (1982), Fabian (1986), Mbaabu (1991), Legere (1992), Karangwa (1995)... Bila kurudia mambo ambayo wamezungumzia tayari na tena vizuri, makala hii ina nia ya kuleta mwanga pale itakapotakiwa na kuonyesha:

- (i) Jinsi historia ya watu wanaozungumza Kiswahili ilivyoathiri historia ya lugha hiyo
- (ii) dhima ya lugha hiyo katika nyanja mbalimbali za maisha ya Waswahili na, yaani wale wote wanaozungumza Kiswahili barani Afrika, bila kusahau hadhi yake, dhana hizo mbili zikiingiliana na kutegemeana kwa namna fulani.

Mkazo utatiliwa hasa sehemu Kiswahili kilipoenea mwisho yaani Afrika ya kati. Upwa wa Afrika Mashariki umezungumziwa ya kutosha na ukitajwa itakuwa kama kweli ni muhimu.

## **1.0 Utukufu wa Kiswahili**

### **1.1. Chombo cha kupigania Uhuru**

1945: Vita vya pili vya dunia vimemalizika. Wakati nchi za Magharibi zinapojipangusa majivu na kujengwa upya, Afrika inaamka pole pole na kuanza kuwaza juu ya mustakabali wake. Inaungwa mkono na mapendekezo yaliyotolewa katika mkutano wa mwaka wa 1945. Sera ya ukoloni inaanza kuchambuliwa na wakoloni na watawaliwa kupitia viongozi wake (Kwame N'krumah, Julius K. Nyerere, A. Sekou Touré, J. Kenyatta...) na mawazo na habari zinavyozunguka ndivyo upepo wa uhuru unavyovuma bila kujali bendera za mataifa hayo ya kimagharibi zinazopepea juu ya nchi za Afrika. Miaka kumi na mitano baadaye nchi nyingi zitakuwa zimepata uhuru.

Umuhimu wa Kiswahili kama chombo cha kupigania ulijitokeza katika vita vya pili vya dunia wakati askari kutoka Afrika Mashariki walipokuwa wakipinga ufashisti hasa hapo Kusini Mashariki mwa Asia. Gazeti *Askari* lilichangia sana kusambaza lugha hiyo na kuifanya ijulikane zaidi miongoni mwa wapiganaji hao. Waliporudi nyumbani baada ya vita hivyo wakawa vyombo vya kuieneza pia katika maeneo walikotoka, pawe mjini au vijijini. Wakaanza kukitumia ili kuwaelezea wenzao visa vyao, maarifa yao na kusambaza dhana za uhuru na kujitegemea ambazo wenyewe walikuwa wakipigania. Hayo yote yalichangia

katika kuhamasisha wananchi na kupalilia njia ya vyama kama TAA<sup>1</sup> iliyogeuka baadaye TANU<sup>2</sup> mwaka 1954. Kiswahili kiliambatanishwa pole pole na uzalendo na utafu. Kama ishara ya ukombozi, kilikuwa kinyume ya Kiingereza ambacho kilionekana kama chombo cha unyanyasaji na ukandamizaji. Baada ya kuwa uti wa mgongo wa kueneza ukoloni, sasa kilisaidia kuupinga. Na utamaduni fulani wa kisiasa, ambao ulikuwa mpya kabisa ulikuwa umeanza kuota.

Magazeti na fasihi zilichangia pia sana katika kueneza lugha na kuamsha kisiasa umma. Mnamo miaka 1950, takribani magazeti arobaini yalikuwa yakitolewa. Mengi yake yalikuwa ya serikali na sauti yake, na mengine yalihaririwa na wamisionari au watu binafsi (Whiteley, 1969:62).

Wakati huo redio kama *Sauti ya Dar es Salaam* na *Sauti ya Mvita* (Mombasa) zilitangaza vipindi vilivyosikika Afrika Mashariki na sehemu za Maziwa Makuu. Mmoja kati ya wajibu wake ulikuwa kuzuia mawazo ya kimapinduzi yaliyoenezwa na *Sauti ya Cairo* (Misri). Upane wa fasihi kulitokea tena ari ya kuandika. Majina maarufu kama vile Shaaban Robert, Mathias Mnyampala, Amri Abedi, Saadani Kandoro na wengi wasiojulikana sana walianza kutunga hadithi fupi, riwaya na diwani za mashairi zilizozungumzia siasa au na masuala mengineyo ya kijamii<sup>3</sup>.

Hivyo, katika miaka ya mwisho ya ukoloni, Kiswahili kilikuwa kinazungumzwa na karibu nusu ya watu wa Tanganyika na hakuna lugha nyingine iliyokuwa na nafasi kama yake katika kuhamasisha na kupitisha propaganda za kupigania uhuru. Julius K. Nyerere, mwenyekiti wa TANU na baadaye raisi wa Tanzania huru mwenyewe katika ziara zake zote nchini alitumia mkalimani mara mbili tu (Whiteley, 1969:65).

Nchini Kenya Kiswahili hakikusambazwa kama vile Tanganyika. Hata hivyo, kama vile Tanganyika, mwamko wa kisiasa ni fursa ya kupima umuhimu wake na umaarufu wake. Tayari katika robo ya kwanza ya karne wafanyakazi wa mijini walikuwa wakikitumia kama lugha ya kupinga unyanyasaji waliofanyiwa. Mfano ni migomo dhidi ya *kipande* iliyoongozwa na Harry Thuku mwaka 1922 (Mkangi, 1985:337). Lakini, uasi mkubwa Kenya ni ule wa Mau Mau ambao ulianza mwaka 1952. Baada ya uhuru Wakenya walifafanua kizalendo maneno hayo kama *Mzungu Arudi Ulaya Mweusi Apate Uhuru*. Hili laweza kufanya mtu awaze kuwa uasi huo ulitumia Kiswahili lakini sivyo. Walioanzisha walikuwa Wakikuyu na neno lenyewe latokana na Kikuyu<sup>4</sup>. Kama Kiswahili kilitumiwa si kwa wingi

---

<sup>1</sup> Tanganyika African Association

<sup>2</sup> Tanganyika African National Union

<sup>3</sup> Taz. Mulokozi (1982)

<sup>4</sup> Kwa mujibu wa Kariuki (1963 :50-51), watoto Wakikuyu wanapocheza hubadili maumbo ya maneno. Neno *uma* maana yake nenda. Badala ya *uma* linakuwa *mau* na hata unaporudiarudia neno hilo utajikuta unatamka Mau Mau. Na katika mkutano mmoja wa siri waasi walikuwa wameahidiana kutamka *Mau Mau* ili watoroke wakiona polisi wanakuja. Ilitokea hivyo na polisi waliposikia Mau Mau wakadhani kuwa lilikuwa jina la kundi hilo. Waasi wenyewe hawakujiita hivyo, wengine ndio waliowapachika jina hilo.

sana, matumizi yake yalilenga kuyahusisha makabila mengine ilipotakika. Baadaye vyama vyote vya siasa, vikubwa vikiwa KANU na KADU, vilizingatia Kiswahili hata kama kutokana na maslahi za kila chama, mitazamo ilibadilika kidogo baadaye na ikabidi lugha za kikabila zitumiwe (Whiteley, 1969:68). Kwa mujibu wa Chimera (1998:91-92), sababu yake ni kwamba Kenya ilipopata uhuru ilikuwa bado na matatizo ya kuunda umoja wa kweli wa kisiasa, na Wakenya walikuwa bado na kinyongo mbele ya Wazungu na mambo yao yote. Ni mojawapo ya sababu za kutokiendeleza Kiswahili.

Nchini Kongo mawazo ya uhuru yalianza miaka ya 1950 hivi na kufika upeo wake miaka mitano baadaye kina P. Lumumba, M. Tshombe, J. Kasavubu na wengineo walipotambuliwa kama viongozi halisi wa vuguvugu hilo. Hao wote walitumia Kifaransa kwa sababu walihutubia hasa utawala wa kikoloni na jamii ya kimataifa. Ila hawakuwa na budi kutafsiri ujumbe wao kwa wenzao Wakongo. Na hapo waliweza kuchagua katika lugha za kikabila au lugha ya Kifaransa. Kutumia lugha ya mkoloni halingekuwa jambo la busara tena kwa sababu mbili. Mosi, ilibidi pawe na mkalimani na, kwa kawaida shughuli ya ukalimani huwa haikosi kasoro, na kama wasemavyo Waitalia *traduttore traditori*, mkalimani msaliti. Katika muktadha wa kuhamasisha watu, kuwahutubia kwa lugha yao mama ndiyo njia hasa ya kupasha kweli ujumbe wenyewe na kuungana nao kikwelikweli. Lakini dosari yake ni kwamba unapodai muungano na umoja wa wananchi, si busara kuanza kuleta tofauti tofauti kati ya watu. Na hapo ndipo matumizi ya lugha isiyodaiwa kuwa ya kabila fulani, inakuwa jawabu la maana na uamuzi bora.

Katika sehemu kunakozungumzwa Kiswahili kulitokea vyama vitatu vya kisiasa : MNC<sup>5</sup> yenye makao makuu Stanleyville<sup>6</sup> (Kisangani), CONAKAT<sup>7</sup> Elisabethville (Lubumbashi) na CERE<sup>8</sup> Bukavu. Waanzilishi wake walikuwa P. Lumumba<sup>9</sup>, G. Munongo<sup>10</sup> na A. Kashamura na J. C. Weregemere. Kutokana na malengo ya kila chama, mwenendo wake katika mambo ya lugha ulijidhihirisha.

---

Katika lahaja za Kiswahili za Rwanda, Burundi na Uganda neno *maumau* lina maana ya jambazi, mhuni.

<sup>5</sup>Mouvement National Kongolais.

<sup>6</sup>Ninaacha makusudi majina ya miji na nchi kama yalivyokuwa yakitumiwa nyakati zinazozungumziwa.

<sup>7</sup>Confédération des Associations tribales du Katanga

<sup>8</sup>Centre de Regroupement Africain

<sup>9</sup>Lumumba alizungumza vizuri Kiswahili. Mulokozi ([www.helsinki.fi/hum/aakkl/documents/kiswahili.pdf](http://www.helsinki.fi/hum/aakkl/documents/kiswahili.pdf)) anatoa mfano wa namna alivyosaidia wenzake wapigania uhuru kutoka Afrika Magharibi ambao hawakujua Kiingereza na wale wa Afrika Mashariki ambao hawakujua Kifaransa, walipokutania kwa Sekou Touré mwezi Mei 1959. Alitumia Kiswahili kuwasiliana na wale wa Afrika Mashariki na kutafsiria wengine kwa Kifaransa kabla ya kutafsiri kauli zao kutoka Kifaransa hadi Kiswahili.

<sup>10</sup> Munongo ni mjukuu wa mtemi Msiri ambaye alikuwa amezaliwa Unyamwezi mwaka 1830. Alikuwa amehamia sehemu za Kusini Mashariki mwa Kongo mwaka 1858 na baada ya kuuu mfalme wa mahali hapo, akaanzisha ufalme unaojulikana kama Ufalme wa Gareganze. Munongo hataongoza kwa wakati mrefu chama cha CONAKAT kwa sababu uongozi wake utakabidhiwa M. Tshombé.

MNC ilinuia kuwa na wafuasi nchini pote na hapo ilikipendelea Kifaransa kuliko lugha za kikabila au Kiswahili ambacho kilionekana hasa kama lugha ya majimbo ya Mashariki. CEREAL ilitumia Kiswahili na Kifaransa kwa sababu Bukavu ni mahali pa Kiswahili. Ila chama hicho hakikudumu kwa sababu kiligeuka tawi la MNC mjini Bukavu.

CONAKAT hutoa mfano mzuri unaolingana na mada yetu kwa kuwa inakusanya vyama vingi vidogo vya makabila mbalimbali ambavyo havingelifika mbali kama visingelijiunga pamoja. Katika propaganda zake na mikutano yake, CONAKAT ilitumia Kiswahili (Polomé, 1982:369). Pia Kifaransa na Kiflemishi vilikuwa vinaweza kutumiwa kwa sababu kulikuwa na Wabelgiji wengi sehemu hizo za migodi. Chama cha CONAKAT kiliwakusanya watu wanaozungumza Kiswahili na kiliwasaidia kupambana na watu wa kabila la Waluba waliokuwa wanatoka jimbo la Kasai na ambao walikuwa na nguvu zaidi. Baadaye Waluba hao walijiunga na CONAKAT ili waweze kupingana na vyama vikubwa kama MNC na ABAKO<sup>11</sup> vilivyokuwa Stanleyville na Leopoldville (Kinshasa). Na Kiswahili kikawa lugha ya mawasiliano kwao wote.

Katika mwaka wa 1959 hivi, vyama hivyo vya kisiasa vilitumia Kifaransa kwa ajili ya Wazungu na wageni kwa ujumla. Lakini vilitumia zile lugha tatu muhimu kwa ajili ya wenyeji; ABAKO ilitumia Kikongo, MNC Ki-Lingala na Kiswahili<sup>12</sup> na CONAKAT Kiswahili. Lugha hiyo iliendelea kutumika kama chombo cha kuwaunganisha wananchi wa sehemu hizo dhidi ya mkoloni hata kama haikuwa rahisi kama tutakavyoona baadaye.

Katika harakati hizo za kupigania uhuru, kando ya vyama vya kisiasa vilivyojulikana Kongo pia kulikuwa na chama cha kimasiya (messianic) kilichojulikana kwa jina la *Kitawala*<sup>13</sup>. Neno hili ni namna ya kibantu ya kusema *Watch Tower*, madhehebu yaliloanzishwa huko Marekani mwaka 1874 hivi na mtume Ch. Russel. Madhehebu haya yaliingia Afrika kupitia nchi za Liberia, Nigeria na Afrika ya Kusini. Yalifika Kongo kutokea nchi hiyo ya mwisho kupitia Rhodesia (Zimbabwe) na Zambia na ni fundi seremala anayeitwa Mwana Lesa ambaye alikuwa ameyaeneza madhehebu haya huko Kongo tangu 1923. Kwa kufanya ufafanuzi huru wa Biblia, madhehebu haya yalitabiri mwisho wa dunia na kurudi kwa Yehova duniani. Yehova angebomoa utawala uliokuwepo ambao ni wa Shetani na kuanzisha serikali inayoongozwa na Mungu (Theocratic). Wafuasi wa Kitawala walibadilisha ujumbe na kuutumia kisiasa wakiwaza kuwa siku za heri ni zile mkoloni Mbelgiji atakapofukuzwa. Hawakupenda wageni na walianza

---

<sup>11</sup> Association des Bakongo pour l'Unification, la Conservation, le Perfectionnement et l'Expansion de la langue Kikongo.

<sup>12</sup> Stanleyville, makao makuu ya MNC, ni mji ulioko katika sehemu ya Ki-Lingala na Kiswahili. Ila ni Kiswahili kilichotumiwa sana pale katika harakati za kisiasa. Wakazi wenye asili ya kiarabu na wengine kutoka sehemu za Maniema waliunga mkono chama hicho. Na ukabila uliwafanya Watetela wamuunge mkono ndugu yao Lumumba wakisaidiwa na majirani zao Wakusu. Waislamu – wanaozungumza Kiswahili – hutoka kwa wingi katika makabila hayo mawili. Gazeti la chama hicho lilikuwa linaitwa *Uhuru*.

<sup>13</sup> Taz. Fabian (1971)

kutumia nguvu na kuwatesa watu kabla ya kupigwa marufuku na utawala wa kikoloni. Vita vya pili vya dunia vilisaidia chama hicho kuenea katika sehemu ya Kusini na Mashariki mwa Kongo, kutoka Elisabethville hadi Stanleyville (Cornevin, 1989:222).

Katika miaka 1950 wakoloni na watu wa dini waliambatanisha chama hicho na wazungumzaji wa Kiswahili na kuwashtaki kuwa ndio walikifanya kiachane na mawazo asilia ya *Watch Tower* na kuwa Kitawala. Kwa mujibu wao, neno hilo lilimaanisha “utawala”, majilio, kutokana na shina “-tawal- ambalo halina la kufanya na *Watch Tower*, hata kama Kiswahili kilisaidia chama hicho kusambaa.

Baada ya uhuru wa Kongo (Juni 30 1960), nchi hiyo haikuishi katika usalama na utulivu kwa sababu ya nia za kujitenga za sehemu zake nyingi. Ndoto yake ya kuwa huru, kama nchi nyingi barani Afrika, ilitekelezwa kabla ya umoja wa kisiasa kufikiwa. Na, kama tutakavyoona baadaye, uasi wote ulitokea katika sehemu za Mashariki na Kusini ambazo lugha yake ilikuwa Kiswahili.

Visiwani Komoro Kiswahili hakikuzungumzwa lakini kilikuwa na dhima fulani kabla ya uhuru. Katika miaka ya 1960, Wakomoro waliokuwa wakiishi Tanzania waliunda chama cha ukombozi wa Komoro (MOLINACO) na walikuwa wakitumia redio Tanzania kutoa ujumbe wao wa kisiasa kwa Kiswahili na Kikomoro<sup>14</sup>.

Uhuru wa nchi ya Msumbiji ulipatikana baada ya vita na wapigania uhuru wa FRELIMO ambao wengi wao walipata mafunzo ya kijeshi nchini Tanzania. Hatuna ushahidi kama walikitumia Kiswahili baadaye katika kampeni zao za kivita ila mchango wake ni dhahiri.

## **1.2. Chombo cha ukombozi**

Baada ya uhuru, maeneo ya mapigano ambapo Kiswahili kilitumiwa ni katika nchi mbili hasa, yaani Uganda na Rwanda.

Uganda ilipata uhuru wake bila harakati kubwa kama nchi nyingine za Afrika Mashariki. Nchini humo Kiswahili kilijulikana kama lugha rasmi ya wanajeshi tangu zama za ukoloni. Pale ambapo hakikutumika kupigania uhuru, kilijitokeza kama chombo cha “kukomboa” Uganda chini ya utawala wa kidikteta wa Idi Amin Dada aliyekuwa madarakani tangu 1971. Kampeni zote za ukombozi tangu 1978 zilitokea Kusini mwa nchi hiyo na kuungwa mkono na Tanzania. *Bakombozi*<sup>15</sup> wote, wawe wa chama cha UPC<sup>16</sup> cha M. Obote au wa NRA<sup>17</sup> wa Y. Museveni walitumia Kiswahili katika shughuli zao za kijeshi.

---

<sup>14</sup> Moja kati ya matokeo yake ni maneno mengi ya mkopo kuingia katika Kikomoro, hasa katika nyanja za utawala na nadharia ya kisoshalisti (Omar, 1995 : 103).

<sup>15</sup> Wakombozi katika lugha za kibantu za Uganda.

<sup>16</sup> Uganda People’s Congress

<sup>17</sup> National Resistance Army

Kufanikiwa kwa operesheni hiyo kuliwapa baadaye mawazo wakimbizi Wanyarwanda ambao walikuwa wakiishi Uganda na waliowahi kujiunga na *Bakombozi* au waliotumikia jeshi la Uganda. Mwezi Oktoba 1990 walivamia Rwanda wakisaidiwa na Uganda lakini hawakufanikiwa moja kwa moja kufika Kigali na kupindua serikali ya J. Habyarimana. Uasi huo uliendelea mpaka 1994 ambapo waliweza kuingia madarakani baada ya kukomesha mauaji ya halaiki. Wao walichagua mapema kutumia Kiswahili kwa sababu mbili. Mosi, waliojiunga na uasi huo walikuwa wanaishi katika nchi za Afrika Mashariki kunakozungumzwa Kiswahili. Lakini pia kulikuwa na wakimbizi kutoka Kongo, Burundi na pia watu wengine kutoka Rwanda. Kuchagua Kifaransa au Kiingereza haingewezekana, wote hawakuwa na ujuzi wa kutosha wa lugha hizo. Kinyarwanda kingeweza kuwaunganisha lakini wote hawakukijua vizuri kutokana na kuishi kwa muda mrefu uhamishoni. Pili, kulihitajika tofauti kati yao na wanajeshi wa Rwanda ambao walitumia Kinyarwanda na Kifaransa. Na katika mapigano ya 1994, ili kuwatambua wenzao vitani walitumia Kiswahili, na adui alitambuliwa kuwa ni yule ambaye hakuweza kujibu maswali yao kwa Kiswahili. Na hata leo amri za jeshi la Rwanda zinaendelea kutolewa kwa Kiswahili. Na hadhi ya Kiswahili imepanda zaidi kwa sababu watu walikiona kama lugha ya ukombozi wao (Ntakirutimana, 2002:121).

Kushadidia wazo hilo, Ntawigira (1997:78) aliandika :

Leo Kiswahili ni lugha ya usalama, lugha inayotumiwa na walinzi wa nchi na usalama wa Wanyarwanda, yaani wanajeshi. Mnyarwanda asiyejua Kiswahili anajitahidi kuelewa na kujifunza lugha hiyo ili aweze kuwasiliana vizuri na wanaochunga usalama wetu... Lugha ya Kiswahili inaonekana kama lugha ya wakombozi wa nchi. Kutokana na hayo; watu wengi wanajifunza lugha ili wavae nao sura hiyo nzuri. Kiswahili ni dalili ua ushujaa, uangalifu, uungwana na busara.

### **1.3. Kiswahili na utaiifa**

Vita vya Maji Maji (1905-1907) ni tendo la kwanza mwanzoni mwa karne lililosaidia Kiswahili kuenea na kujaribu kukifanya kiwe lugha ya taifa, hata kama wazo hilo lilikuwa halijasambaa sana, kwani vita hii ilihusisha makabila karibu ishirini na sehemu kubwa ya Tanganyika. Naam, tukio hili lilisaidia kufuta mageuzi na sheria za unyanyasaji wa wakulima. Lakini pia lilikuwa muhimu kwa sababu lilionyesha Watanganyika kuwa wangeweza kuivuka mipaka ya ukabila na lugha na kujenga kundi la maana kisiasa. Mbegu hiyo ilikua vizuri na kusaidia katika harakati za kupigania uhuru na hasa baadaye katika siasa ya Ujamaa, na hata leo. Kila siku Kiswahili kilichukuliwa kama nguzo ya utaiifa na utekelezaji wa uhuru kupitia lugha na hatua ya kujitoa kweli katika ukoloni<sup>18</sup>.

Baada ya kuupata uhuru wake, Kenya haikubadili sera iliyoachwa na wakoloni ambayo ilikuwa kama piramidi iliyo na Kiingereza juu, Kiswahili katikati na lugha za kikabila chini. Hali ya Kiswahili katika nchi hiyo ilidhihirisha msimamo

---

<sup>18</sup> Dhima ya lugha imezungumziwa kwa mapana na marefu na Whiteley (1969), Abdulaziz (1971), Massamba (1986), Crozon (1998)...

wa watawala wake ambao walikuwa wanavutwa kati ya hadhi ya juu ya Kiingereza, umuhimu wa kisiasa na kijamii wa Kiswahili na kutosahau lugha zao za kikabila. Kukikuzi na kukiendeleza Kiingereza kama lugha rasmi kulikuwa rahisi kuliko kuchukua lugha yoyote nyingine. Mfumo wa siasa ambao ulikaribia zaidi ubepari unaeleza jinsi ilivyokuwa vigumu kutozingatia lugha hiyo. Ushirikiano na Uingereza uliendelea kuimarika na ulikuwepo hasa kupitia sekta ya uchumi ambayo ilikuwa mikononi mwa masetla wa zamani na Wahindi. Lugha hiyo ilisaidia kuunganisha watu hao wachache na wenye uchumi mikononi mwao ambao ndoto yao huendelea kwa kupitia lugha yenyewe.

Mabadiliko – angalau madogo lakini ya maana – yalitokea mwaka 1969. Mosi katiba ilibadilishwa kidogo na kifungu chake kimoja kikasema kuwa ujuzi wa Kiswahili ulikuwa wa lazima kwa yeyote atakayeomba uraia wa Kenya. Lakini vile vile, vifungu vingi vilithibitisha Kiingereza kama lugha pekee ya majadiliano Bungeni, na yule asiyekijua hakuweza kugombea ubunge (Gorman, 1974 : 438). Mbaabu (1985:190-191) hutoa mfano wa mbunge aliyekosa nafasi yake aliposhindwa zoezi la Kiingereza. Pili Kamati Kuu ya chama tawala Kenya African national Union KANU, kilikitambua Kiswahili kama lugha ya taifa la Kenya. Kukubaliwa huko kulikipa Kiswahili msaada rasmi na wa kiitikadi ambao kiliukosa tangu miaka kadhaa. Uliwafanya Wakenya wapate hisia ile ya utaiifa wa kilugha na magazeti yakapokea kwa mikono miwili habari hiyo. *Daily Nation* ya Aprili 8 1970 iliandika (ikinukuliwa na Whiteley, 1973:14) kwamba:

“Swahili shall be spoken at all times, whether officially or unofficially, politically or socially. Official language in all Government duties will be conducted in Swahili. All civil servants in all governmental, quasi governmental, diplomatic services, etc. will have to pass both oral and written Swahili tests... All non citizens who will apply for citizenship... shall prove orally or by writing... that they are capable of conducting a meaningful conversation in Kiswahili. Failure in Kiswahili will be automatic disqualification for citizenship”.

Makala nyingine hazikukosa hisia za uasi dhidi ya Kiingereza na *hegemonia* yake. Rhoades (1977:2-3) anatoa mfano katika gazeti *Taifa* la Mei 23 1970 :”Mwananchi anayependelea Kiingereza zaidi ya Kiswahili inafaa asafiri hadi Uingereza...”. Onyo hili lilikuwa likiyarudia vikali maneno ya Mzee J. Kenyatta katika mkutano wa hadhara na wananchi Mombasa hapo Agosti 31 1969 ambapo alisema:

“Whether some people will like my decision or not Kiswahili will be spoken in our Bunge ... because it is the language of the Wananchi... English is not our language and the time will come when we will do everything in Swahili. I know that many people will be annoyed, but let them.”(*East African Standard* ya Septemba 1 1969 ikikiriwa na Heine, 1990:45).

Matunda ya kampeni hiyo yalipatikana mwaka 1974 Kiswahili kilipoteuliwa kuwa lugha ya Bunge. Matumizi ya Kiswahili yalileta dukuduku juu ya ujuzi wa

wabunge katika Kiswahili. Kwa wengi wao kufuta Kiingereza kulimaanisha kuangamia kisiasa kwao na kupoteza athari yao ambayo waliitunza vizuri kwa lugha hiyo inayoeleweka kwa watu wachache sana (Mazrui na Zirimu, 1978:450; Mbaabu, 1985:190-192). Kutokana na mashinikizo ya kisiasa (Heine, 1990:180), Kiingereza kilijipatia tena nafasi yake kama lugha pekee mwaka 1978. Mwaka huo ndipo alifariki Mzee J. Kenyatta ambaye aliamini kwa dhati uwezo wa Kiswahili na kujaribu kukisaidia kuenea kweli kwa kutumia upendo na umaarufu wake katika mioyo ya wananchi.

Hata kama Kiswahili hakiungwi mkono rasmi, kinabaki katika mawazo ya Wakenya kama “lugha ya kila mtu, ya kazi, ya watu” (Heine, 1990:180) na kuwa ni uti wa mgongo wa utaiifa. Kama anavyoandika Kanuri (1992:91-92), malengo ya mafunzo ya Kiswahili Kenya ni kuimarisha umoja wa taifa na usawa wa kijamii wa wananchi wote.

Nchini Uganda, Kiswahili kilingoja mpaka Idi Amin Dada<sup>19</sup> awe madarakani ili kuweza kuteuliwa kama lugha ya taifa katika agizo la rais la Agosti 7, 1973. Uamuzi huo ulikuwa matokeo ya mijadala mirefu tena mikali iliyoyagonganisha majimbo yaliyounga mkono Kiswahili na Luganda. Majimbo kumi na mawili ya Wanilotiki na ya Kaskazini yaliunga mkono Kiswahili na majimbo manane ya Kusini kunakozungumzwa lugha za kibantu yalikipendelea Kiganda. Walakini sheria hiyo haikufuatiwa na hatua ambayo ingeiweka kweli katika matendo na mpaka leo, isipokuwa kukisikia redioni na katika televisheni<sup>20</sup>, kukiona juu ya shilingi na vyapa fulani barabarani, hakuna uwanja rasmi ambapo kinatumiwa.

Kiswahili kuwa chombo cha utaiifa Uganda ni kama ndoto za mchana. Kasoro kubwa kwake ni kutokuwepo kabila fulani la kijamii lenye nguvu ambalo lingetambulika kwa Kiswahili<sup>21</sup>. Katika karne moja na zaidi, Waganda walikiona Kiswahili kama kifaa tu bila kukitambua kamwe kama sehemu, kipengee cha urithi, mali yao ya taifa na kitamaduni. Na jambo hili hueleza vizuri jinsi watu hawaitikii hata kidogo mapendekezo na maagizo yanayotolewa na serikali zinapotaka kiwe lugha ya taifa. Zote zinasahau kuwa lugha hiyo ni ya kigeni, ililetwa Uganda na ni vigumu kuiona ikimaanisha kweli utamaduni na utaiifa wa Uganda.

Tangu mwanzoni mwa karne ya 20, Kongo nayo inakumbana na tatizo la kuchagua lugha moja ya taifa kati ya lugha nne kubwa za taifa ambazo ni Kikongo, Tshiluba, Ki-Lingala, na Kiswahili. Jambo linaloshangaza ni kwamba mijadala kuhusu lugha ya taifa<sup>22</sup> iliyofanywa enzi za ukoloni haikuzingatia hata kidogo Ki-Lingala, ambayo ilikuwa lugha rasmi ya jeshi tangu mwisho wa vita

---

<sup>19</sup> Inasemekana kuwa alipokuwa rais alikuwa anazungumza vizuri na kwa ufasaha Kiswahili kuliko Kiingereza (Scotton, 1972:23).

<sup>20</sup> Taz. Balinda na Ruhangalinda (1995).

<sup>21</sup> Mfano wa kampeni ya Baganda kukikuza na kukiendeleza Kiganda (Mukama, 1991:337-340 na 343).

<sup>22</sup> Mjadala mkubwa ulifanyika mwaka 1944, Taz. *Bulletin de l'Institut Royal Colonial Belge*, 15/2, 1944.



vya kwanza vya dunia<sup>23</sup>. Hadhi yake ilipanda mwishoni mwa miaka 1950 watu kutoka Kaskazini Magharibi mwa Kongo walipohamia kwa wingi katika mji mkuu Leopoldville. Hapo ndipo ilipoanza kuwa lugha ya mji mkuu na hasa lugha ya wanamuziki karibu wote wa Kongo. Kiswahili kilikuwa na turufu nyingi lakini kikaachwa kwa sababu baadhi ya wapinzani wake walidai kuwa hakikuwa lugha halisi ya Kongo kama vile Tshiluba na Kikongo ambazo kasoro zake zilikuwa kutojulikana sana na kufungamana na ukabila. Sababu nyingine ilitokana na kuona Kiswahili kama chombo cha Uislamu na hali Kongo ilikuwa mikononi mwa Wakatoliki kwa kiasi fulani. Na huu ulikuwa ni unafiki mtupu kwa sababu watu hao wa dini walikuwa wanakitumia Kiswahili hicho kuhubiri neno takatifu na serikali ilikuwa inakitumia kuendeleza siasa nake. Baada ya uhuru, ili kupambana na umajimbo, ukabila na majanga yote yanayobomoa umoja wa taifa, Kifaransa ndicho kilichotangazwa kama lugha rasmi ya Kongo na lugha zile nne zikatangazwa zote kama lugha za taifa katika majimbo zilipozungumzwa.

Miaka michache baada ya Mobutu kushika madaraka mwaka 1965, alianzisha mapinduzi ya kitamaduni yaliyojulikana kwa neno la Kifaransa *authenticité* yaani kujaribu kuwa Mwafrika, hasa Mkongo halisi anayeheshimu mapokeo na anayejivunia asili yake bila kuiga wageni kwa ujumla na hasa Wazungu. Lakini la kuchekesha ni kwamba mambo hayo yote yalifanyika kwa Kifaransa, lugha ambayo haina unasaba na Uafrika. Swali la lugha moja kwa ajili ya taifa likazuka na kama kawaida halikupata jawabu. Ila ufundishaji wa lugha zile katika shule ya msingi<sup>24</sup> ukafufuliwa. Hata kama lugha zote zilikuwa za taifa, moja ilikuwa ya taifa zaidi. Ki-Lingala, ambayo ni lugha ya Mobutu na ndugu zake wengi waliokuwa madarakani, ilionekana kwa kiasi fulani kama lugha ya taifa lote. Siasa yake ya *authenticité* alikuwa akiitoa mahali popote kwa Ki-Lingala na watawala wote, ili kurahisisha mambo au kulinda maslahi yao, waliitikia wito wa Mkuu wao. Itikadi iliyoongoza Kongo – *Umobutu* – ikasikika zaidi na vizuri kwa Ki-Lingala. Hadhi ya Ki-Lingala ndivyo ilivyopanda na mwaka 1976, Bokamba (1976) alipojadili katika makala yake juu ya uchaguzi wa lugha ya taifa katika muktadha wa *authenticité* alionyesha kuwa Ki-Lingala na Kiswahili ndizo lugha muhimu zilizoweza kupigania nafasi ya lugha ya taifa<sup>25</sup>. Alionyesha jinsi Ki-Lingala kilivyokuwa na bahati nyingi<sup>26</sup> za kuchaguliwa kama lugha ya taifa. Hata hivyo alionyesha kuwa ukizingatia bajeti, uchaguzi wa Kiswahili ungeweza

---

<sup>23</sup> Kabla kuundwa kwa Jeshi la Kongo kulikuwa askari wa kukodiwa kutoka Afrika Magharibi (Nigeria, Ghana, Liberia) na Afrika Mashariki (Ethiopia, Somalia, Zanzibar). Wa kwanza walitumia Kihansa na wengine Kiswahili. Walipoondoka Kiswahili kiliendelea kutumiwa katika majimbo ya Mashariki na Katanga kama lugha ya kufundishia maaskari wa Kongo. Ki-Lingala kilitumiwa mahali pengine pote na baada ya 1914 ndipo ilikuwa lugha rasmi ya Jeshi popote Kongo.

<sup>24</sup> Baada ya uhuru, serikali mpya ilitaka watu wote wasome Kifaransa kwa kupinga sera ya kikoloni ambayo iliwanyima Wakongo uwezo wa kusoma sana Kifaransa na kwa Kifaransa.

<sup>25</sup> Kwa mujibu wa Edema (2000:60), Ki-Lingala huzungumzwa na watu milioni 10 hali Kiswahili ni milioni 12. Katika uchunguzi alioufanya mjini Kinshasa juu ya lugha ambayo ingekuwa lugha rasmi ya Zaïre, wahojiwa wa Baibanja (1978:199) walikipendekeza Kiswahili kwenye nafasi ya kwanza (52.5%) mbele ya Ki-Lingala (42.4%) na Tshiluba (3%). Kikongo hakikutajwa.

<sup>26</sup> Lugha ya mji mkuu, kuwepo kwa walimu, lugha ya jeshi, lugha ya muziki, lugha halisi ya Kongo...

kurahisisha mambo na kugharimu pesa chache. Pia aliongezea kuwa ingekuwa faida kubwa kwa Zaïre kwa sababu Kiswahili kingesaidia Zaïre kukaribiana kisiasa na kiuchumi na nchi nyingi za Afrika Mashariki (Bokamba, 1976:39-40). Lakini hayo yote yalikuwa mapendekezo tu na hakuna lililofuatia.

Hali ilibaki ile ile mpaka Mobutu alipotolewa madarakani na L.D. Kabila mwaka 1997. Rais huyo, ambaye alisaidiwa na Wanyarwanda na Waganda kupindua serikali ya Mobutu, alikuwa ameishi uhamishoni kwa miaka mingi Afrika Mashariki. Pia alikuwa mzaliwa wa Katanga na uhusiano wake na Kiswahili haukuwa wa jana wala juzi. Alipofika madarakani alitaka kufuta kwa hima kila kitu kilichoweza kukumbusha *umobutu*. Baadhi ya mambo aliyoyafanya ni kujaribu *kukisukuma* Kiswahili, lugha iliyomaanisha ushindi, ukombozi na kupinga udikteta. Kiswahili kilikuwa ishara ya mambo yote mapya, kinyume na Ki-Lingala kilichokuwa ishara ya *umobutu* na maovu yote aliyotendea nchi yake. Kulitokea hatua za uelekeo huo na zenye uzito fulani na ambazo hata Mobutu mwenyewe hakuthubutu kufanya. Timu ya soka ya taifa ilibatizwa *Simba* badala ya *Léopards*<sup>27</sup>, pasipoti ya Kongo ikaandikwa kwa lugha tatu (Kifaransa, Kiingereza na Kiswahili), noti mpya zikawa na Kiswahili juu yake. Hayo yote yanaonyesha nia<sup>28</sup> aliyokuwa nayo Kabila, ambaye alianza kujulikana kwa Wakongo wote kwa jina la *Mzee*.

Lakini awe ni Kabila au mwingine, Wakongo kwa ujumla huwa na picha nzuri ya Kiswahili. Katika uchunguzi alioufanya Nkongolo (1998) mjini Kinshasa<sup>29</sup>, Kiswahili kinapewa nafasi ya kwanza kama lugha ya fahari, tajiri na iliyoenea sana Kongo. Pia kinapendekezwa mbele ya lugha nyingine za taifa kama lugha inayoweza kusaidia kujenga umoja wa Wakongo.

#### **1.4. Kiswahili kama ishara ya ustaarabu na usomi**

Ujuzi wa Kiswahili ulikuwa na maana tofauti kulingana na mahali kilipotumiwa Afrika Mashariki, au ya sehemu za Maziwa Makuu. Ni dhahiri kuwa mwanzoni mwa karne ya 20 kwa ujumla kujua Kiswahili kulikuwa ufunguo wa kisomo, kuweza kuelewa ustaarabu na utamaduni mwingine na mpya. Mambo hayo ambayo baada ya muda yalikuwa ni ya kawaida Afrika Mashariki (hasa Tanganyika), sehemu za Ruanda-Urundi yalionekana kama fahari kubwa sana. Shule za watoto wa watemi na watawala wa enzi hizo zilikuwa zikitoa masomo yake kwa Kiswahili na wafalme Musinga (1896-1931) wa Ruanda na Mutaga (1908-1915) wa Urundi walisoma hesabu na kuandika kwa Kiswahili. Na Kiswahili kilikuwa kigezo kikubwa cha kutathmini watawala wa Kinyarwanda. Usipojua lugha hiyo ulionekana vibaya kwa serikali ya kikoloni ambayo ilipendelea zaidi lugha hiyo kuliko Kinyarwanda na Kirundi ambazo zilikuwa ngumu kusoma. Wazungu na baadhi ya Warundi waliwaita kwa chuki *Bashenzi*,

---

<sup>27</sup> Mnyama ishara (TOTEM) ya utawala wa Mobutu.

<sup>28</sup> Kwa kukiendeleza Kiingereza na Kiswahili Kongo, wachunguzi waliona nia ya L.-D. Kabila ilikuwa kuivuta nchi yake kuelekea zaidi kiuchumi na kisiasa Afrika Mashariki na ya Kusini. Kwa mfano, Kongo iliingia moja kwa moja katika Jumuiya ya SADEC (Southern African Development Community).

<sup>29</sup> Eneo ambalo kwa kawaida halina watu wengi wanaozungumza Kiswahili.

*Wabirimani*<sup>30</sup> au *ng'ombe ya Mwambutsa*<sup>31</sup> wale wote ambao hawakujua Kiswahili. Na mtu kutojua lugha hiyo hakueleweka na kukatokea msemu wa “*Nutazi igiswahili ntayoberwa na ndiyo*”, yaani, “Hata kama hujui Kiswahili basi usikose kujua *ndiyo*.” Baada ya 1929, Kiswahili kilitolewa katika ratiba za shule na nafasi yake ikachukuliwa na Kifaransa. Lakini kizazi kilichokisoma kiliendelea kujivunia ujuzi huo maadamu waliojua Kifaransa hawakuwa wengi. Kiliendelea kuwa ishara ya ustaarabu katika sehemu fulani kati ya Unyarwanda au Urundi halisi na uzungu uliopitia Kifaransa.

Dhana ya uungwana na walioitwa waungwana Mashariki mwa Kongo inaingia katika mkondo huo. Mwanzoni waliojiita waungwana ni watoto na wajukuu wa wachuuzi wa Kiarabu au chotara kutoka Tanganyika na Zanzibar ambao walihusika na biashara ya watumwa na madini. Walijiita waungwana wakitaka kujitofautisha na washenzi. Baadaye jina hilo lilipewa pia weusi ambao walisilimu na kuishi pamoja na waungwana hao. Nguzo mbili ziliwaainisha: Kiswahili<sup>32</sup> na Uislamu. Na ni dhahiri kuwa mambo hayo mawili yaliwasaidia kuerevuka na kustaarabika kuliko Wakongo wa kawaida. Biashara iliwasaidia pia kuwa na uhusiano na wenzao wa Afrika Mashariki.

Mpaka mwanzoni mwa karne ya 20, Kiswahili kilikuwa lugha ya mawasiliano katika baadhi ya miji ya pwani Mashariki mwa Madagaska. Kilikuwa kinazungumzwa na wahamiaji kutoka Unguja au Komoro. Dhima yake ilikuwa ile ya “lugha ya uhusiano wa kimataifa (mikataba), biashara na ubaharia, na fasihi fulani<sup>33</sup> (Guenier, 1987:72). Kiswahili kilififia pole pole baada ya kuenea kwa Kifaransa na kupungua kwa uhusiano wa kibiashara katika sehemu hiyo ya Bahari ya Hindi. Mwishoni mwa miaka 1990, *Kosahily*<sup>34</sup> kilikuwa kinazungumzwa na watu wazima wachache ambao walikaa katika miji hiyo ya Kiswahili ya zamani. Leo vijana hawakijui hata kidogo.

### **1.5. Kiswahili na umajimbo**

Sura hii ya Kiswahili ilijitokeza baada ya uhuru, zaidi nchini Kongo na kwa kiasi fulani nchini Sudan. Tangu enzi za ukoloni kulikuwa na mvutano kati ya watu kutoka Kaskazini Magharibi mwa Kongo na wale wanaotoka katika majimbo mengine. Na ilitokea kuwa wa kwanza ndio waliokuwa wengi katika utawala mjini Kinshasa. Uhusiano kati ya makundi hayo ulikuwa wa ushindani na kuchukiana kiasi kwamba Waswahili walikuwa wakiwaita *Batoka chini* (Fabian, 1986:42-43).

---

<sup>30</sup> Kifupisho cha “Washenzi wa vilimani”.

<sup>31</sup> Mwambutsa ni mfalme wa zamani Burundi (1915-1966).

<sup>32</sup> Neno Kingwana lilipewa na baadhi ya wakoloni wa kibelgiji lahaja ya Kiswahili inayozungumzwa Kongo. Lakini ukweli ni kwamba neno hilo lina maana tu mtu anapozungumzia Wangwana, halitumiwi na halijulikani kwa Wakongo ambao hudai kuzungumza Kiswahili.

<sup>33</sup> Ushairi wa kifalme katika kasri ya wafalme wa Madagaskar.

<sup>34</sup> Wamadagaskar hukiita hivyo Kiswahili !

Kutangazwa kwa uhuru wa Katanga siku kumi na moja tu<sup>35</sup> baada ya uhuru wa Kongo ilikuwa moja kati ya dalili za mzozo huo. Serikali hiyo tenganifu ikachagua Kifaransa na Kiswahili kama lugha rasmi. Kando ya Katanga makundi mbalimbali yaliwania madaraka pia katika majimbo ya Mashariki. Kwa mfano kundi la waasi waliojiita Simba<sup>36</sup> na baadaye uasi ulioongozwa na askari wa kukodiwa Mbelgiji J. Schramme. Ni wakati huo ambapo pia kina L. D. Kabila na Che Guevara<sup>37</sup> walishirikiana ili kujaribu kupindua serikali ya Kinshasa. Uasi huo wote uliachia Kiswahili picha ya lugha ya kimapinduzi ambayo iliambatana na uasi na kuvuruga hali iliyokuwepo. Na pia kuliundwa pamoja na lugha hiyo wazo la alama ya kijimbo ambayo ilitaka kupinga wale waliokuwa Kinshasa na kuzungumza Ki-Lingala. Tangu wakati huo mpaka leo Kiswahili kiliimarisha wazo hilo la watu wa sehemu za Mashariki na kuwa chombo cha hisia zao kama watu kutoka majimbo hayo.

Nchini Sudan, lugha ya Kiswahili hujulikana katika jimbo la Equatoria. Na uhusiano huo na Kiswahili unatokana na kwamba jimbo hilo ni karibu na Kongo, Uganda na Kenya. Kwa mujibu wa Mahmoud (1982:161), watu wachache sana wanadai Kiswahili kama lugha-mama yao. Lakini inajulikana zaidi miongoni mwa vijana ambao kwao ni ishara ya usasa na inadalilisha ndoto zao zote kuhusu Afrika ya Mashariki (Miller, 1984:47). Umuhimu wake kama lugha ya jimbo hilo ulijitokeza mwanzoni mwa miaka 1980 wasomi wa Equatoria walipoanzisha kampeni ya kutafuta lugha ya jimbo lao la Kusini mwa Sudan. Katika harakati za kupambana na Sudan Kaskazini yenye utamaduni wa kiislamu na kiarabu, walipendekeza Kiswahili, Kiingereza na lugha moja ya kikabila ili moja kati ya hizo ichukue nafasi ya Kiarabu. (Miller, 1984:40). Suala hilo lilijadiliwa kwa wakati mrefu katika magazeti ya hapo. Na makala hizo zote zilifuatana na *Make Swahili the National Language*, makala iliyokuwa imeandikwa na Sir Anai Kelueljang katika gazeti la *Nile Mirror*. Labda mjadala huo unaendelea na hasa kwa sababu bado wakimbizi wengi wapo Uganda na Kenya<sup>38</sup>.

## **2.0 Upande mwingine wa sarafu : Kiswahili lugha mbaya**

Nimechagua kichwa hiki kidogo cha *Kiswahili lugha mbaya* ili kuonyesha umuhimu wa maoni ya watu juu ya lugha. Maoni hayo ambayo yanaanza yakiwa ya kibinafsi wakati mwingine huenea katika jamii nzima na hata kuathiri mtazamo wa watawala. Hisia ya kuona Kiswahili kama lugha isiyofaa ilianza enzi za ukoloni na kuendelea hata baada ya uhuru. Ilichangiwa na wakoloni na baadhi ya Waafrika wenyewe. Sababu na hoja zilitofautiana kutoka kundi hadi jingine.

---

<sup>35</sup> Julai 11 1960.

<sup>36</sup> Uasi huo ulitokea Uswahilini Maniema na mbinu zao hukumbusha vita vya Majimaji kwa sababu walijipaka dawa na kuamini kuwa itazigeuza risasi za adui maji ; Haikuwa hivyo !

<sup>37</sup> Che Guevara na waasi wenzake kutoka Cuba na penginepo walijiita majina ya Kiswahili (Moja, Mbili, Bendera, Agano...) ambacho kilikuwa lugha ya operesheni za kivita na mawasiliano ya kawaida. Che Guevara mwenyewe aliitwa Tatu.

<sup>38</sup> Sudan People Liberation Army ina ofisi yake mjini Nairobi.

## 2.1. Wakoloni dhidi ya Kiswahili

Baada ya Kiswahili kusaidia kusambaza itikadi ya ukoloni kwa mafanikio, wakoloni wenyewe walikuja kugundua kuwa kingeweza kuwa kipingamizi cha maana kwa maslahi yao na lengo lao ambalo lilikuwa kujenga “*civilised East Africa, based upon the British ideas, British language, British culture, and British institutions...*” (Legere, 1987:155). Kisingizio rasmi kilikuwa kwamba Kiswahili kilikuwa “*...weak in its powers of expressing European ideas*” na kuwa na “*limitations as a language*” (Ripoti za Utawala wa Waingereza zikikaririwa na Legere, 1987:155).

Usambazaji wa Kiingereza ungesaidia kuunda wananchi ambao wangukuwa watumishi waaminifu wa utawala wa kikoloni na hivyo kupinga mwamko wowote wa kisiasa ambao ungepashwa vizuri kwa wananchi wote kupitia Kiswahili au lugha za kikabila. Ndivyo Kiingereza kilivyoungwa mkono nchini Kenya na Uganda kuanzia mwaka 1950.

Katika makoloni ya Ubelgiji, tangu mapema sera ilikuwa kutowafundisha Waafrika Kifaransa au Kiflemishi. Kwa mujibu wa Alexandre (1967:114), ilikuwa njia nzuri ya kuwafungia Waafrika katika jela ya lugha za Kiafrika tu ili kuwalinda wasisome mambo mabaya. Fabian (1986:57) anakiri maneno ya kamishna mmoja wa jimbo ambaye alipokuwa anajadili maneno ya mtumishi wake mmoja alisema:

*“The quintessence of his documented exposé is : teach the Black to read French and he will give himself over to revolutionary and pornographic French papers and he will be after the novels and other immoral books published in the French language. And this gentleman concludes : go on teaching French to the Negro and you’ll morally destroy the race while at the same time preparing the revolution which will chase you - which, by the way, is what you deserve. –I share this view”.*

Ndiyo maana Kiswahili – kama vile lugha nyingine za Kiafrika - kwa upande huo hakikuwa na matatizo mengi hasa nchini Kongo.

Kwa baadhi ya wakoloni Kiswahili kilikuwa kizuri, kasoro yake kubwa ilikuwa kuambatanishwa kwake na “balaa” mbili kwa mfumo wa ukoloni : Uislamu na ukomunisti. Mpaka wakati huo Uislamu ulikuwa tishio kwa, hasa, wamisionari Wakatoliki<sup>39</sup>. Na ulipoingia ukomunisti, tishio likahusu mfumo wote wa kikoloni. Mawazo ya uhuru yaliungwa mkono na mikutano ya Bandung (1955) na Accra (1958), na watu wa Afrika waligundua kuwa matarajio yao yaliambatana na aina ya ukomunisti wa kiAsia ambao ulikuwa unalenga uhuru wa nchi zilizotawaliwa na wakoloni kutoka Ulaya. Nchi za kiarabu zilikuwa na dhima kubwa katika harakati hizo. Wabelgiji wakaanza kushuku kuwa Waarabu, Wahindi na Wapakistan, ambao walikuwa Afrika Mashariki, wangeleta mawazo hayo Kongo na Ruanda-Urundi kupitia njia ulipopitia Uislamu na wafanyabiashara Waarabu. Njia hizo hazikutumia Kiarabu, bali Kiswahili. Mwezi Agosti 1955, Mfalme

---

<sup>39</sup> Hata kama dini zote za kikristo zilikutumia Kiswahili kuhubiri !

Seoud wa Saudi Arabia, A. G. Nasser wa Misri na waziri mkuu wa Pakistan walikutania Mecca na kuunda programu ya kueneza Uislamu Afrika. Wakati huo *Sauti ya Cairo* (Misri) na *Sauti ya Afrika Huru* ya Radio Delhi (India) zikaongezea vipindi vya Kiswahili kwa ajili ya Afrika Mashariki na ya kati. Kamati kuu ya Waislamu ikaanzishwa na makao makuu yakawa Dar es Salaam, wakati ambapo ng'ambo radio Zanzibar ilirusha vipindi vya Redio Cairo. Mwanzoni propaganda zilikuwa za kidini. Lakini mara kwa mara viungo vya itikadi ya kisiasa viliongezewa. Waislamu, wasikilizaji wa kwanza wa ujumbe huo, hawakukaa kitako tu. Na kinyume na wenzao wa Afrika Mashariki ambao hawakujali sana mijadala ya kisiasa, Waislamu wa Afrika ya kati wao walivutiwa na mambo hayo na kujihusisha sana. Stanleyville, mji wa P. Lumunba na makao makuu ya MNC, ukawa mbele katika propaganda hizo zote.

Kwa wakoloni, mahali Kiswahili kilipoenea palikuwa pia mahali Waislamu walipoenea. Kwa hiyo Kiswahili kiliwasaidia kueneza propaganda na kilikuwa chombo mwafaka kwa wakuu wa dini na wanasiasa wageni kutoka Afrika Mashariki. Ili kukomesha mambo hayo, hatua zikachukuliwa kufundisha Kifaransa badala ya Kiswahili ili kumwezesha Mwafrika kuijua lugha hiyo ambayo ilikuwa chombo cha ustaarabu na utamaduni wa Wabelgiji (Bannouet, 1981:16).

Mambo yalivurugika pia Rwanda baada ya uhuru (1962) makundi ya wakimbizi yalipoanza kushambulia Rwanda kutoka Uganda, Burundi na Kongo. Enzi hizo kulikuwa na shauku na hofu ya kuwa wakimbizi hao wataunda chama cha wachochezi wa kisiasa na kuvuruga hali ya amani. Kwa mujibu wao, bila shaka wangetumia Kiswahili badala ya Kinyarwanda<sup>40</sup>.

## **2.2. Waafrika dhidi ya Kiswahili**

Kupinga Kiswahili kutoka kwa Waafrika wenyewe kulitokana na sababu mbalimbali, kukiwemo kulinda maslahi ya makabila au makundi fulani na kukiona kama lugha ya unyanyasaji.

### **2.2.1 Kulinda maslahi za kabila au kundi fulani**

Jambo hili hupatikana hasa Uganda ambapo kabila la Baganda lilikuwa na uwezo mwingi kisiasa, kijamii na kiuchumi tangu enzi za ukoloni. Waingereza walipofika Uganda walishirikiana na Baganda kueneza matakwa ya serikali na siasa yao, Kiganda kikaenea hivyo na wakajipatia uwezo namna hiyo. Wamisionari wakaanza kutumia Kiganda badala ya Kiswahili kilichokuwa kimetumiwa awali kuenezea Ukristo na, hasa, Uislamu. Baganda na wamisionari waliafikiana kupambana na Kiswahili ambacho kilihatarisha maslahi yao ya kisiasa na kidini. Wengine walitaka kuimarisha umuhimu wao juu ya makabila mengine ambayo yangesaidiwa na Kiswahili kujiunga dhidi yao na wengine walitaka kulinda nchi hiyo ya Kikristo dhidi ya athari za Uislamu. Mkataba huo ulidumu na Kiswahili hakina njia thabiti ya kushamiri nchini humo ingawa watawala wa kikoloni walikuwa na ari ya kukifanya kiwe lugha ya nchi. Na

---

<sup>40</sup> Utabiri huo ulikuja kutokea mwaka 1990.

mambo yalichacha serikali ya kikoloni ilipobadili msimamo wake na kukataza walowezi Wazungu kuja tena Uganda na kuwapa wakulima, hasa Baganda na Wahindi, mashamba ya mazao ya kuuza nje. Kila jaribio la kuendeleza Kiswahili liliwekewa kura ya turufu ya Baganda ambao walihofu kuwa ilikuwa hatua ya kuiunganisha nchi yao na Kenya na kuwafanya wapoteze faida zao zote.

Nchini Kenya kabila la Waluo lilihofu Kiswahili kwa sababu kingepunguza hali yao kikiunganisha na makabila mengine ambayo yanazungumza lugha za kibantu. Miongoni mwa wanaozungumza lugha hizo, Wakikuyu na Wakamba walitia viziwi kwa maendeleo ya Kiswahili. Hoja zao zilikuwa kwamba lugha hiyo haikuwa ya taifa kuliko Kikuyu, Kikamba au lugha nyingineyo yoyote ya Kenya. Walitaja athari za Kiarabu katika Kiswahili na kuonyesha kuwa hakikuwa lugha ya Kiafrika na kibantu halisi. Na, kwa hakika, wengine walikiona kama Kiarabu (Chimerah, 1998:94).

### **2.2.2. Hatari kwa lugha na tamaduni za kikabila**

Kuenea kwa Kiswahili kunasababisha kwa kiasi fulani kutoendelea na kutokua kwa lugha ndogo ambazo hatimaye zinaweza hata kufifia pamoja na tamaduni zinazozitumia kama chombo.

Enzi za ukoloni nchini Tanganyika kwa makabila makubwa kama vile Wahaya, Wasukuma, na Wachaga Kiswahili hakikuwa kimeenea vizuri japo kuna wakati kuliwahi kuwa na aina ya “upinzani” dhidi ya lugha hiyo. Upinzani huo ulidhihirika kwa kuanzishwa kwa magazeti katika lugha za kikabila kama vile *Ng’hulu ja Basukuma* Usukumani na *Bukya na Gandhi* Uhayani<sup>41</sup>. Magazeti haya hayakudumu muda mrefu kwa sababu wasomaji walipendelea zaidi Kiswahili katika muktadha wa kujenga umoja wa taifa. Lakini hata hivyo dhana ya alama na kutosahau wala kupoteza asili yao haikufutika. Kwa mfano katika miaka 1990, majilio ya demokrasia yalifufua kwa namna fulani mawazo hayo. Bila kutangaza wazi ukabila wake, vyama vilichimbuka vya kutetea na kuleta maendeleo ya watu kutoka sehemu, tarafa au mkoa fulani au kuonyesha wazi mwelekeo wao. Mfano unatolewa wa kufufuliwa kwa magazeti ya zamani *Rumuli* na *Lumuli* Uhayani na Usukumani (Batibo, 1992:94-96). Kudumisha na kuziendeleza lugha za kikabila si jambo lililokubaliwa na wote kwa kuwa kwa wengi ilimaanisha ukabila na tishio kwa umoja wa taifa.

Huko Kongo pia enzi za ukoloni baadhi ya watu walikuwa na hofu kuwa lugha zao zingemezwa na Kiswahili (Kyatangala, 1957:690). Wengine walianza kuwakatisha tamaa wale waliotaka kusoma Kiswahili (Makonga, 1953:46).

Hisia hiyo ilikuwepo pia Rwanda katika miaka 1978. Wakati huo Kiswahili kilikuwa kinaanza kufundishwa tena na watu wengi kujiandikisha katika masomo yake. Wasomi wengi wakaanza kukumbuka Unyarwanda wao na kuanza kuutetea. Katika mikutano au kwa maandishi wakaonyesha tishio kubwa la uwili-lugha wa Kiswahili-Kinyarwanda, na hatari ilikuwa kubwa zaidi kwa sababu lugha

---

<sup>41</sup> Taz. Legere, 1986, 159-160 na 163.

zenyewe ni dada. Hofu yao ilikuwa kwamba Kinyarwanda kingemezwa iwapo hali ingeendelea hivyo (Bangamwabo, 1986). Na, kama anavyosema Ohly (1982:107), Kiswahili pia ni:

*...language of an elaborated ideology represented within the language by specific vocabulary, hence, the geographical spread co-incides with geopolitics. And that is the heart of the matter: as Swahili is not a 'nobody' language, so it is not an 'everybody' language. Language cannot be completely neutral: something of the culture, attitudes and habits of thought it describes will influence somehow those who speak it."*

Kando ya kumezwa kwa lugha, walihofu pia dhana za kisiasa zilizoambatana na lugha ya Kiswahili. Woga wa aina hiyo haukuwa Rwanda tu. Mbaabu (1991:115-116) anataja hofu ya utawala wa kilugha na kitamaduni ambao ulikwenda sambamba na Kiswahili cha Tanzania. Anakiri kuwa: "maoni ya Wakenya wengi kwamba Kiswahili cha Tanzania kimeathirika sana kwa kutumia istilahi nyingi za kisiasa na kitaaluma ambazo matumizi yake ama hayajakolea, au yanaegemea siasa za upande mmoja..." na kutoa mfano wa fasili inayotolewa na Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI, 1981:94)<sup>42</sup> kwa neno "kabaila" ambayo inafungamana sana na propaganda ya kijamaa.

Misimamo hiyo yote huonyesha wazi kuwa kustawi kwa Kiswahili ni lazima kuzingatia kuwepo kwa lugha nyingine na kuheshimu haki ya kila lugha kuwepo kwani zote ni ya taifa na dunia.

### **2.2.3. Chuki ya Kiswahili**

Mwenendo wa wazungumzaji wa lugha fulani au hadhi yao katika jamii huathiri sana maoni ya watu wengine kuhusu lugha hiyo. Chuki ya Kiswahili inatokana na sura za namna mbili ambazo ziliambatana na Kiswahili : lugha duni na lugha ya ukandamizaji.

#### **(i) Lugha duni au iliyodunishwa**

Nchini Rwanda, na kwa namna fulani Burundi, Kiswahili kilinasibishwa na Waislamu na Uislamu. Dini hii ilikuwa adui kwa dini ya Kikatoliki ambayo ilifanya iwezavyo ili kuizuia kuenea. Katika kampeni hiyo ya kuupinga Uislamu Kiswahili nacho, kama lugha ya kusambazia dini hiyo, kikaonwa vibaya. Waislamu<sup>43</sup> wapakachikwa picha hiyo ya watu duni, walaghai na wadanganyifu<sup>44</sup>. Lugha yao ikachukuliwa vile vile kama lugha duni na isiyo na thamani yoyote<sup>45</sup>. Vizazi vingi vilikua vikiwa na wazo hilo potofu. Kwao mtu aliyezungumza Kiswahili alionekana kama mtu asiye na kisomo kwa kumlinganisha na yule

---

<sup>42</sup> Na chapa nyingi zilizofuata karibu kila mwaka.

<sup>43</sup> Si kusema kwamba wao ndio pekee waliokuwa hivyo, udanganyifu na ulaghai unapatikana kwa binadamu yeyote na haufungamani na dini wala kabila...

<sup>44</sup> Ili kuonyesha kuwa ulikuwa mgogoro wa kidini, watu kutoka Kongo waliozungumza Kiswahili hawakuchukiwa sana na Wanyarwanda au Warundi. Tatizo lilizuka watu wale walipokuwa na majina ya Kiislamu kama vile Juma, Hamis, Ibrahim, Shabani n.k.

<sup>45</sup> Katika Kinyarwanda *kubwira umuntu igiswahili*, kumwambia mtu Kiswahili ni kumwambia uongo, kutumia sababu za uongo au visingizio ili uepuke hali mbaya uliyomo.



ambaye alikuwa amesoma Kifaransa. Na hapo tunafikia dhana ya Kiswahili kama lugha ya kabwela, lugha ya malaya na lugha ya ukandamizaji na unyanyasaji.

**a) Lugha ya kina kabwela**

Wazo hili lilienea zamani Rwanda, Burundi, Uganda na Kenya hata kama leo linaanza kufifia katika nchi zile mbili za kwanza. Uganda Kiswahili kilidharauliwa hasa na Baganda wanaokiita *lulimi lwa kipakasi* (Kawoya, 1985:76), yaani lugha ya wapagazi waliofanya kazi katika mashamba ya Baganda na Wahindi katika Ufalme wa Buganda<sup>46</sup>. Hali i vile vile Kenya ambapo mawazo hayo hayakubadilika sana tangu enzi za ukoloni. Kama zamani Kiswahili kilichukuliwa kama lugha ya maboi, leo kinaonekana kama cha makabwela wa ngazi ya chini hasa kwa wale waliobahatika kuwa na kisomo ni wale wenye kujua na kutumia Kiingereza (Chimerah, 1998:92).

**b) Lugha ya malaya**

Jambo hili lilikuwa la ukweli kwa sababu katika nchi hizo umalaya<sup>47</sup> ulikuwa mijini na kando kando ya barabara kuu kwenda bandari ya Mombasa wakati ambapo wateja walikuwa madereva wa malori au wageni kutoka Kongo au Afrika Mashariki ambao walizungumza Kiswahili kama lugha ya mawasiliano. Na lugha hiyo iliwasaidia sana katika kazi hiyo ambayo kwa wenzao ilikuwa ya aibu<sup>48</sup>.

**c) Lugha ya ukandamizaji na unyanyasaji**

Popote Kiswahili kinapasibishwa na ukandamizaji ni baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe au baada ya mapinduzi ya tawala.<sup>49</sup> Mwenendo wa majeshi nchini Uganda baada ya Kabaka kutolewa madarakani mwaka 1966 haukusaidia sana kuleta picha nzuri ya Kiswahili nchini humo. Mazrui na Zirimu (1978:444) wanatoa mifano ya mateso na unyanyasaji wa watu ambao hatia yao ilikuwa kutojua vizuri Kiswahili. Waliposimamishwa kwenye viziwi vya barabarani waliulizwa maswali kwa Kiswahili na adhabu ililingana na kiwango chao cha Kiswahili. Majeshi, ambayo wengi wa askari wake walitoka sehemu za Kaskazini, yalitumia lugha hiyo kama mbinu ya kulipiza kisasi na kuwakomesha hasa Baganda ambao walikuwa na matatizo ya kisiasa nao.

Miaka kumi na zaidi baadaye majeshi kutoka Tanzania pamoja na Waganda walimfukuza Idi Amin Dada na kuikomboa nchi. Kiswahili kilionekana kama lugha ya ukombozi na kikaitwa na Baganda *Kikombozi*. Lakini baadaye kulitokea vitendo vya uhalifu na vya uovu vilivyofanywa na majeshi au watu wengine

---

<sup>46</sup> Kuanzia miaka 1945 hadi miaka 1970 watu wengi kutoka Ruanda-Urundi na Tanganyika walihamia Buganda kwenda kutafuta kazi na pale walizungumza Luganda kama lugha ya kuwaingiza (to integrate) katika jamii ya Baganda na Kiswahili kama lugha mawasiliano kati ya watumishi wengine Waafrika.

<sup>47</sup> Katika Kinyarwanda na Kirundi malaya ni *indaya* au *malaya*.

<sup>48</sup> Mpaka leo kwa mfano Burundi wanaona kuwa ni jambo la kawaida kwa mwanamme kuzungumza Kiswahili lakini kwa mwanamke si vizuri (Karangwa, 1995 :232).

<sup>49</sup> Ila ni Burundi. Nchini humo kwa baadhi ya watu wazima Kiswahili kiliwakumbusha enzi za ukoloni na mateso yake, ukali wa watumishi wa kikoloni kutoka Kongo na kazi za kulazimishwa walizofanya. Hayo yote yalifanywa kwa Kiswahili.

waliokuwa wakitumia Kiswahili na kwa dharau neno *Kikombozi* likawa na maana kutoka Kiganda yaani lugha ya wanyang'anyi, wakora na wanyakuzi (Snoxall, 1985:15 na 24). Picha hiyo mbaya hutunzwa mpaka ndani ya michezo ya kuigiza. Mukama (1995:14) anataja kuwa katika michezo hiyo Kiswahili “chaingizwa tu kuhusiana na uhalifu, ujambazi na unyama”.

Nchini Rwanda pia wale ambao hawakupenda Kiswahili chuki yao iliongezewa na maneno ya Kiswahili waliyoyasikia baada ya mauaji ya halaiki ya 1994. Wengi wao walichukia sana sentensi kavu “*wewe mtu gani ?*” ambayo ilikuwa sentensi ya kwanza ya wanajeshi walipoomba raia wajitambulishe. Hitayezu (1999:82) anazungumzia hali hiyo ifuatavyo: “Ukweli ni kwamba utakuta baadhi ya wanajeshi wakiambia watu wasiojua Kiswahili mambo kama ‘kuja hapa, wewe mtu gani’. Jambo hili huzuia mawasiliano na kumchanganyikisha (sic) msikilizaji au kumtisha”. Na mara nyingi wasiopenda lugha hiyo hubaki na picha yake kama “lugha ya kutisha na ya matusi” (Hitayezu, 1999:18). Balinda na Ruhangalinda (1995:41) wanasema kuwa amri za “*Fungua mlango, Kaa chini*” wanazozitamka majambazi wakati wanapovamia raia ni sababu mojawapo za watu wa wilaya za katikati mwa Uganda kukipinga Kiswahili.

Kama tulivyoona awali, nchini Kongo, baada ya L.D. Kabila kupindua serikali ya Mobutu, Kiswahili kilipewa hadhi fulani. Lakini kuswahilisha huko kwa nchi kulifanywa kwa ghafla na kwa nguvu, bila kura yoyote ya maoni ya wananchi. Ni dhahiri kuwa Wakongo wote hawaridhiki kwa sababu hatua hiyo ni kinyume na demokrasia. Mabana (2002) anaandika kuwa Kiswahili kilikuwa kinatawala katika ofisi zote za serikali Kinshasa na katika mikutano isiyo rasmi. Na, kwa mujibu wake, ingekuwa vizuri lugha zote za taifa zipewe nafasi sawa. Hali hii inamfanya mwanaisimujamii Edema (2000:67) ajiulize litakalotokea kesho mtu kutoka Kasayi anayezungumza Tshiluba au Bandundu na anayezungumza Kikongo atakaposhika madaraka. Na Edema huyo huyo aliniambia<sup>50</sup> kuwa hali hiyo ya kuwaona Waswahili kwenye vyeo vyote huwafanya wawachukie na wachukie lugha yao. Kwa mujibu wake kuna mzozo kati Waswahili wenyewe: Waswahili kutoka Katanga ambao wana vyeo muhimu vyote na wale kutoka sehemu nyingine ambao wanatengwa na kujikuta wakisingiziwa makosa ya utawala wa leo Kinshasa. Na hayo yote huharibu kwa kiasi fulani sura ya Kiswahili kwa Wakongo wasiokizungumza<sup>51</sup>. Kinachukuliwa na baadhi yao kama chombo cha udikteta mpya ambao umechukua nafasi ya ule wa Mobutu na lugha yake ya Ki-Lingala.

---

<sup>50</sup> Mazungumzo kwa simu ya Mei 30 2003.

<sup>51</sup> Kwa kawaida mjini Kinshasa, kama alivyoambiwa Baibanja (1978 :277), Kiswahili kilionekana kama lugha nyororo, yenye heshima na adabu kwa sababu ya mwenendo wa wazungumzaji wake. Hapo walikilinganisha na lugha ya Ki-Lingala ambayo kwa maoni yao haina heshima wala adabu (chuki ya majeshi na wenyeji wa Kinshasa) na Tshiluba ambayo hunasibishwa na ukabila na kujiona kwa Waluba.

### 3. Hitimisho

Makala hii imejadili jinsi maisha na historia ya watu na nchi kunakozungumzwa Kiswahili zilivyoathiri lugha hiyo katika karne ya 20. Yametoa picha muhimu mbili za Kiswahili, yaani picha nzuri, tukufu na nyingine inayokionyesha katika hali mbaya. Juu ya picha ya kwanza Kiswahili kilionekana kama lugha inayonasibishwa na dhana za uzalendo, uhuru, usomi, na kupigania haki za binadamu kwa ujumla. Picha ya pili ilikionyesha katika hali yake duni kama lugha ya makabwela; wakati mwingine inaambatanishwa na hatari kwa lugha nyingine au binadamu mwenyewe kama chombo cha uhalifu na mateso kwake. Pamoja na hayo tumeona jinsi dhima na hadhi ya lugha huathiriana katika maendeleo na ukuzaji wake. Hatuwezi kudai kuwa mada yenyewe, ambayo ni pana, tumeichunguza katika pembe zake zote. Lengo letu lilikuwa kutoa angalau picha ya kijumla juu ya mambo ambayo bila shaka yanastahili kufanyiwa uchunguzi zaidi.

### Marejeo

Abdulzaziz, M.H., 1971, "Tanzania's National Language Policy and the Rise of Swahili Political Culture", katika W.H. Whiteley, (mh.), *Language Use and social change : Problems of multilingualism with special reference to Africa*, London: OUP, kur.12-18.

Alexandre, P., 1967, *Langues et langage en Afrique noire*, Paris: Payot

Baibanja, K., 1978, *La situation sociolinguistique à Kinshasa*, thèse de 3ème cycle, Univ. d'Aix Marseille I.

Balinda D. na Ruhangalinda, 1995, "Sera ya Matumizi ya Kiswahili Uganda", katika S.A.K. MLACHA, (mh), kur.. 38-48.

Bangamwabo, F.X., 1986, "Les problèmes du bilinguisme au Rwanda : situation actuelle", CIRELFA, *Aménagement linguistique et terminologique au Rwanda : Bilan et perspectives*, Kigali: Minesupres, kur. 247-267.

Bannout, N., 1981, *L'Islam au Zaïre sous le régime colonial*, Mémoire de DEA, Paris:EHESS

Batibo, H., 1992, "The Fate of Ethnic Languages in Tanzania" katika Brenzinger, M. (mh.), *Language Death : Factual and Theoretical Explorations with Special Reference to East Africa*, Berlin:Mouton de Gruyter, kur..85-98.

Bokamba, E.G., 1976, "Authenticity and the Choice of a National Language : the Case of Zaïre", in *Studies in the Linguistic Sciences*, 6/2, kur.. 23-57.

Chimerah, R., 1998, *Kiswahili : Past, Present and Future*, Nairobi: Nairobi University Press.

- Chiraghdin, Sh. na Mnyampala, M., 1977, *Historia ya Kiswahili*, Nairobi: OUP, Nairobi.
- Cornevin, R., 1989, *Histoire du Zaïre des origines à nos jours*, Bruxelles: Hayez Ed
- Crozon, A ., 1998, “Dire pour séduire : Langages et politique en Tanzanie”, D.C.
- Martin, A. *Nouveaux langages d politique en Afrique orientale*, Paris: Karthala-Ifra, kur. 115-185.
- Edema, A., 2000, “Glottoculture et glottophagie en République Démocratique du Kongo”, A. Lemarechal, *Les langues en danger*, Paris: Peeters, kur.57-77.
- Fabian, J. A., 1971, *Jamaa : A Charismatic Movement in Katanga*, Northwestern Univeristy Press.
- Fabian, J.A., 1986, *Language and Colonial Power : the Appropriation of Swahili in the Former Belgian Kongo 1880-1938*, Cambridge: Cambridge University Press.
- Gorman,, T.P., 1974, "The Development of Langage Policy in Kenya with Particular Reference to the Educational System" katika Whiteley, W. H., (mh.), *Language in Kenya*, OUP, Nairobi, kur.397-479.
- Guenier, N.J., 1989, “Le swahili à Madagascar”, P. Alexandre and M.F. Rombi, *Le Swahili et ses limites : ambiguïté des notions reçues*, Éd. Recherche sur les civilisations / 1989, kur. 179-182.
- Heine, B., 1970, *Status and Use of African Lingua francas*, Munchen: Weltforum-Verlag.
- Heine, B., 1990, "Hali ya Kiswahili kama Lugha ya Taifa", katika K., Legere (Mh.), pp.86-93.
- Hitayezu, T., 1999, *Matumizi ya Kiswahili katika uwanja wa jeshi la Rwanda : Mtazamo wa kiisimujamii*, Butare: Mémoire de Licence, Université Nationale du Rwanda.
- Kanuri, J.M., 1992, “Sera ya uteuzi wa vitabu vya Kiswahili katika shule za msingi nchini Kenya”, katika K. Legere, (mh.), kur. 89-103.
- Karangwa, J. de D., 1986, *Kiswahili katika Uwanja wa Biashara nchini Rwanda : Mtazamo wa Kiisimujamii*, Ruhengeri: Mémoire de Licence, Université Nationale du Rwanda.
- Karangwa, J.de D., 1995, *Le kiswahili dans l'Afrique des Grands Lacs : contribution sociolinguistique*, Thèse de doctorat, Paris: INALCO.

Karangwa, J de D., 1996, "Rwanda : vers une nouvelle politique linguistique ?", katika C., Juillard na L-J, Calvet, *Les politiques linguistiques, mythes et réalités*, Aupelf Uref: FMA.

Kariuki, J. M., 1963, *Mau Mau detainee : the account by a Kenya African of his experiences in detention camps, 1953-1960*, Nairobi: Oxford University Press.

Kawoya, V.F.K., 1985, "Kiswahili in Uganda", J. Maw na D. Parkin (Wah.), kur. 35-45.

Kyatangala, T.R., 1957, "Le Kirega, une langue qui se meurt", *La Voix du Kongolais*, 138, uk. 690.

Ladefoged, P. Na wenziwe, 1972, *Language in Uganda*, London: OUP.

Legere, K. (mh.), 1992, *The role of Language in Primary Education in Eastern Africa with special reference to Kiswahili*, Bonn: DSE-ZED.

Legere, K., 1986, "Kiswahili na Lugha nyingine katika harakati za kudai uhuru Tanganyika (1945-1961)", *Kiswahili*, kur.152-165.

Legere, K., 1990, "Recent Development of Kiswahili (with particular reference to Tanzania)", katika K., Legere, (mh.), kur.50-84.

Legere, K., (mh.), 1990, *The Role of Language in Literacy Programmes with Special Reference to Kiswahili in Eastern Africa*, Goethe Institute.

Mabana, C.K., 2002, "Enjeux politiques actuels en République démocratique du Kongo", *D+C Développement et Coopération*, 1, Janvier/Février 2002, kur. 27-29 (<http://www.dse.de/zeitschr/df102-9.htm#top>)

Mahmud, U., 1982, "Language Spread as a Wavelike Diffusion : Arabic in Southern Sudan", katika R.L. Cooper, *Language Spread: Studies in Diffusion and Social Change*, Bloomington: Indiana University Press, kur. 158-183.

Makonga, B., 1953, "Sur l'avenir du Kingwana", *Aequatoria*, 16, kur. 46-48.

Massamba, D.P.B., 1987, "The Impact of Politics on Language Development in Tanzania", *Kiswahili*, 54/1, kur.180-191.

Maw J. na Parkin, D. (wah.), 1985, *Swahili Language and Society*, Vienna: Beiträge zur Afrikanistik.

Mazrui, A.A. na Zirimu, P., 1978, "Church, State, and Marketplace in the Spread of Kiswahili : Comparative Educational Implications", katika Spolsky, B. na Cooper,

R.L. (ed.), *Case Studies in Bilingual Education*, Rowley: Newbury House, kur.427-453.

Mbaabu, I., 1985, *New Horizons in Kiswahili : a Synthesis in Developments, Research, and Literature*, Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbaabu, I., 1991, *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*, Nairobi: Longman, Kenya.

Miller, C., 1984, *Etude sociolinguistique du développement de l'arabe au sud Soudan*, Thèse de 3<sup>e</sup> cycle, Université Paris III.

Miller, C., 1986, "Langues et intégration nationales au Soudan", in *Politique africaine*, 23, kur..29-41.

Mkangi, K.G.C., 1985, "The Political Economy of Kiswahili : A Kenya :Tanzania Comparison", katika J. Maw na D. Parkin, (wah.), kur. 331-348.

Mlacha, S.A.K., (mh), 1995, *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki*, Dar es salaam: TUKI.

Mukama, R., 1989, "The Linguistic Dimension of Ethnic Conflict", katika Rupesinghe, K. (ed), *Conflict Resolution in Uganda*, Ohio University Press, kur.178-206.

Mukama, R., 1995, "Uendelezaji, Ukuzaji na Usambazaji wa Kiswahili nchini Uganda", katika S.A.K. Mlacha, (mh), kur. 12-25

Mukama, R.G., 1991, "Recent developments in the Language Situation and Prospects for the Future", katika Hansen, H. Na Twaddle E.,M., *Changing Uganda : The Dilemmas of Structural Adjustment and Revolutionary Change*, Nairobi: Heineman, kur..334-350.

Mulokozi, M., 1982. "Protest and Resistance in Swahili Poetry", *Kiswahili* 49/1, kur.25-54.

Ntakirutimana, E ., 2002, *La langue swahili comme base d'unification dans la région des Grands Lacs africains*, Thèse de doctorat, Université de Laval.

Ntawigira, P., 1997, *Kiswahili nchini Rwanda : Mchango katika mradi wa utengenezaji wa siasa ya lugha*, Butare: Mémoire de Licence, Université Nationale du Rwanda.

Ohly, R., 1982, *Swahili, the Diagram of Crisis*. Vienna/Dar es Salaam: AFRO-PUB.

Omar, A.B., 1995, “Utumiaji wa Kiswahili nchini Komoro”, katika S.A.K. Mlacha, (mh), kur. 101-109.

Phillipson, R., 1998, *Linguistic Imperialism*, London: OUP.

Polome, E.C., 1982, *Language, Society and Paleoculture*, Stanford University Press. kur. 25 – 54.

Rhoades, J., 1977, *Linguistic diversity and Language Belief in Kenya: The Special Position of Kiswahili*, Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu (PhD), Syracuse University.

Scotton, C.M., 1972, *Choosing a Lingua Franca in an African Capital*, Edmonton: Linguistic Research.

Snoxall, R.A., 1985, “The East African Interterritorial Language (Swahili) Committee”, katika J. Maw na D. Parkin (wahariri), kur. 15-24.

TUKI (mh.), 1981, *Kamusi ya Kiswahili sanifu*, Dar es Salaam: Oxford University Press.

Whiteley, W., 1969, *Swahili : The rise of a National Language*, London; Methuen & Co Ltd.

Whiteley, W.H., 1973, *To plan is to choose*, Indiana University.

## MAELEKEZO KWA WAANDISHI WA MAKALA

**KIOO CHA LUGHA** ni jarida la Kiswahili la Idara ya Kiswahili linalochapisha makala za fasihi na isimu. Jarida huchapishwa katika **juzuu moja kila mwaka**. Mlenge wa makala ni fasihi na isimu ya Kiafrika. Makala juu ya kipengele chochote cha fasihi au isimu zinakaribishwa, ilimradi ziwe zimeandikwa kwa Kiswahili.

**Makala:** Waandishi wanaombwa kuwasilisha nakala mangu mbili za kila makala na nakalatepe kwa kutumia anwani ya barua-pepe ya Idara: swahili@uccmail.co.tz. Jina la mwandishi, kichwa cha makala, na anwani ya posta na ya barua-pepe viwe kwenye ukurasa tofauti. Makala ziwe zimechapwa kwa kutumia programu ya **Word**, kukiwa na nafasi 2 kati ya mstari na mstari, na kukiwa na pambizo pana pande zote. Ikisiri isiyozidi maneno 150 iwe mwanzoni mwa makala.

Makala ikishapokelewa itasomwa na kutathminiwa na wataalamu wasiopungua wawili kabla ya uamzi kupitishwa kuichapisha. Mwandishi ataarifiwa mara uamzi huo ukishapitishwa.

*Mifano katika makala:* Mifano yote, iwe ya isimu au fasihi, inapaswa ama kuandikwa kwa **herufi koza** au kwa *italiki*, na haina budi kufuatwa na ‘maana’ yake kama inahitajika. Kwa wanaisimu, ishara zinazoruhusiwa ni zile za Alfabeti ya Kifonetiki ya Kimataifa. Iwapo kutakuwa na haja ya kuwa na ishara tofauti ziandikwe kwenye ukurasa tofauti.

*Tanibihi (chini ya ukurasa au mwisho wa makala):* Tanibihi zitumiwe kwa uwekevu; zisiwe nyingi. Kama mwandishi anatumia tanibihi za mwisho wa makala, zichapwe kwenye ukurasa baidi, zikiwa zimeorodheshwa kwa namba.

*Marejeleo:* Utaratibu wa marejeleo uliozoeleka kwa majarida mbalimbali ndio utumike. Kurejelea andiko katika matini kufanyike kwa kuanza na mwandishi, kisha mwaka, na mwisho tarehe, k.m. Mulokozi (1996:35) au (Mulokozi 1996:35).

Mwishoni mwa makala, marejeleo yaliyotajwa katika andiko yapangwe kiabjadi. Majina ya vitabu na majarida yaandikwe kwa *italiki*, nay ale ya makala yawekwe kwenye ‘alama za kufungua na kufunga semi’, kama inavyoonyeshwa hapa:

Mulokozi, M.M. (1996) *Fasihi ya Kiswahili*. DSM: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mekacha, R.D.K. (1997) ‘Disconnecting Education’, katika *Journal of Linguistics and Language in Education*, 3:95-105. DSM: Idara ya Lugha za Kigeni na Isimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

*Majedwali, Michoro, n.k.:* Majedwali, michoro, ramani na picha vipangwe kwa unadhifu kwenye ukurasa. Mahali pa kuweka majedwali, michoro au ramani paonyeshwe kwa uwazi. Majedwali au michoro isiyokaa vizuri kwenye ukurasa mmoja haitachapwa.



**BACK COVER**

ISSN 0856-552 X